# KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC)

# MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPENDEKEZO YA BAJETI YA SERIKALI, 2023/2024 KWA MTAZAMO WA HAKI ZA BINADAMU

Imetolewa Juni 16, 2023

## A. Utangulizi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimefanyia uchambuzi makadirio ya bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka wa fedha 2023/24 kama ilivyo wasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Mh. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Bungeni mnamo tarehe 16 Juni 2023. Katika hotuba hiyo ya mapendekezo ya serikali kuhusu mapato na matumizi, waziri, amependekeza maeneo makubwa ya kibajeti ambayo ni pamoja na;

- Sura ya bajeti;
- Makadirio ya vyanzo vikuu vya mapato;
- Mpango wa matumizi pamoja na mapendekezo ya maboresho ya kisheria.
- Masuala ya kimfumona kiutendaji.

## B. Madhumuni ya uchambuzi

Ni kubaini mwelekeo wa bajeti yenyewe, mambo mapya na yale ya mwendelezo, hatua za kukabili makali ya maisha na mapungufu ya kimfumo yanayokwamisha ukusanyaji mapato, upelekaji wa fedha kwenye maeneo ya matumizi pamoja na yale ya kisheria yanayo hitaji maboresho katika mwaka huu wa fedha.

## C. Lengo la uchambuzi huu

Lengo la uchambuzi ni kuainisha mapendekezo ya kibajeti yaliyo na tija kwa wananchi na kushauri maboresho kwa maeneo yaliyo kwenye hotuba ambayo yana uwezekano wa kuleta masononeko kwa watanzania.

**Uchambuzi huu umezingatia** vigezo vya kimataifa na kikanda vilivyowekwa katika Mikataba mbalimbali ya

kimataifa kuhusiana na maswala ya bajeti kwa mlengo wa kijinsia; haki za binadamu nahususani Mkataba wa kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966, *Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, kijamii na kiutamaduni 1966, Mkataba wa Kimataifa wa kupinga aina yoyote ya Unaguzi dhidi ya Wanawake Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani hususani ule wa malipo halali ya ujira na ule wa mazingira salama na rafiki mahala pa kazi.*

## D. Sura ya bajeti ya Taifa 2023/2024

Bajeti inapendekeza jumla ya **shilingi trilioni 44.39** kukusanywa na kutumika ikilinganishwa na **shilingi trilioni 41.48** kwa mwaka 2022/2023. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa **shilingi trilioni 31.38** sawa na asilimia 70.7% ya bajeti yote wakati mwaka 2022/2023 ilikuwa **shilingi trilioni 28.02** sawa na asilimia 67.5% ya bajeti yote.

- Kwa mwaka 2023/24 Mamlaka ya Mapato (TRA) inatarajia kukusanya shilingi **trilioni 26.73** wakati mwaka 2022/2023 serikali ililenga kukusanya 23.65.

- Mamlaka za serikali za mitaa zinatarajiwa kukusanya shilingi **trilioni 4.66** kwa mwaka 2023/2024 wakati mwaka 2022/2023 Serikali ililenga kukusanya shilingi **trilioni 4.37.**

- Washirika wa Maendeleo wanatarajia kuchangia kwa kutoa misaada na mikopo nafuu yenye jumla ya shilingi **trilioni 5.47** ikilinganishwa na shilingi **trilioni 4.65** kwa mwaka 2022/2023.

i. Serikali inatarajia kukopa **trilioni 5.44** kutoka kwa soko la ndani ikilinganishwa **shilingi trilioni 5.78** kwa mwaka 2022/2023.

ii. Serikali inatarajia kukopa **shilingi trilioni 2.10** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 3.03** kwa mwaka 2022/2023 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara.

### A. Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2023/24

| Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo |
|---|---|
| Shilingi trilioni 30.31 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo trilioni12.77 kwa ajili ya kulipa Deni la Taifa. | Shilingi trilioni 14.08 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo |

### B. Ulinganifu wa bajeti kwa wa fedha 2022/2023 na Mwaka 2023/2024

Tofauti na Bajeti ya mwaka 2022/2023, ambayo iliyojikita;

1. Kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA.
2. Kudhibiti matumizi mabaya ya magari, pikipiki na mitambo ya serikali.
3. Matumizi makubwa ya safari binafsi na zile za kikazi zisizo na tija ikiwemo mtumishi kusafiri kwa ndege huku gari ya serikali ikitangulia kwa njia ya barabara kwa ajili ya mapokezi aendako.

### C. Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 imejikita;

1. Kupunguza kero zinazowakabili wafanyabiashara pamoja na kuendeleza vipaumbele kama ilivyo bajeti ya mwaka 2022/2023.
2. Kuainisha suala la Mabadiliko ya Tabia ya Nchi kama eneo muhimu lenye kuwekewa uzito na Serikali ili kupambana na madhara yatokanayo na mabadiliko hayo.

## D. Vipaumbele vya Bajeti

Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 imeweka vipaumbele vifuatavyo;

a. Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR);
b. Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL);
c. Kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115);
d. Kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (LNG);
e. Kuzalisha umeme wa maji wa Ruhudi (MW 358) na Rumakali (MW 222);
f. Ujenzi wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi);
g. Ujenzi wa barabara na madaraja makubwa;
h. Kuendeleza kanda maalumu za kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo.
i. Pamoja na kuendeleza wekezaji katika kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa makubwa 100.

## E. Masuala ya kijinsia

- Bajeti pendekezwa imeainisha vipaumbele vyake ambavyo vyote vimejikita katika miundombinu. Pamoja na ahadi nyingi hasa katika kukuza masuala ya usawa wa kijinsia bado bajeti hii haijaweka suala hili kipaumbele.
- Tanzania iliweka ahadi kwenye jukwaa la usawa wa kijinsia endelevu (Generational Equality Forum) kuhakikisha maendeleo ya wanawake kiuchumi pamoja na SADC katika kuhakikisha wanatekeleza sera ya jinsia kwa kuweka mifumo bora itakayoipandisha Tanzania kwenye usawa wa kijinsia lakini bajeti hii haijataja ni jinsi gani masuala haya yatatekelezwa na wala bajeti haijatengwa kuweza kuyatekeleza haya.
- Hata katika vipengele vyote vya kiuchumi suala la Jinsia limeachwa nyuma na hakuna mapendekezo ya kimakusudi kukomboa kundi la wanawake lililoko nyuma Zaidi.

- Pamoja na suala la ajira kutajwa kuwaathiri zaidi wanawake kwa mwaka uliopita kwa asilimia 16 dhidi ya wanaume kwa asilimia 8 bado hakuna mkakati wa makusudi ulioependekezwa kwenye bajeti hii utakaowakwamua wanawake na vijana kwenye suala la ajira.
- Mikopo ya Halmashauri iliyosimamishwa kutolewa kwa wanawake, vijana na Watu wenye Ulemavu imeendelea kusitishwa. Na bajeti hii haijatoa suluhisho na wala pendekezo la utolewaji wake hali ambayo bado itaendelea kuwaathiri wanawake ambao mikopo hii imekuwa na faida kubwa sana kwao.
- Pendekezo la kuweka billion 1 kwenye Mfuko wa watu wenye Ulemavu kwa ajili ya kusaidia vifaa ni zuri lakini pendekezo hilo lingezingatia mahitaji hasa baada ya sensa kukamilika na Serikali kutambua idadi ya watu wenye Ulemavu na mahitaji yao. Kiasi cha shilingi billion 1 ni kidogo sana kukidhi mahitaji ya watu wenye Ulemavu ukizingatia kiasi hiki kimewekewa matumizi ya aina mbalimbali ikiwemo kutumiwa na wabunge pamoja na Watoto walio katika mazingira magumu.
- Bajeti hii bado haijaweka taarifa za kijinsia hasa idadi ya watu na asilimia zake ili kuweza kuipa uhai kijinsia. Mfano kwenye mikopo iliyotolewa, huduma za kaya, watumishi waliopandishwa madaraja, walioongezewa mishahara, hata tu idadi ya watu haijatajwa kwa jinsia yaani wanawake, watu wenye ulemavu pamoja na wanaume na vijana bali imetaja kiujumla. Hali hii inafanya mapendekezo yaweze kuacha nyuma makundi mengi muhimu.
- Kwenye masuala ya kidigitali serikali pia ilishiriki katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa kamisheni ya wanawake mwaka 2023 ambapo teknolojia na digitali ilikuwa lengo kuu. Katika mapendekezo ya mwaka huu kwenye digitali na teknolojia serikali haijaonesha ni kwa jinsi gani huduma hizi zitafikia wanawake zaidi amabao ndio wamekuwa nyuma zaidi kiteknolojia na kidigitali ili kuweka usawa wa

kijinsia na kuwakomboa wanawake hasa wa vijijini katika teknolojia na digiti.

### F. Mapendekezo ya kurekebisha sheria mbalimbali

Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 inapendekeza kufanya maboresho katika jumla ya sheria 17 ili kufuta, kupunguza na kuweka tozo mpya katika maeneo mbalimbali ili kukuza uchumi, Sheria hizo ni kama ifuatavyo;

1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;
2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
4. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438; 91
5. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;
6. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, SURA 289;
7. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;
8. Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, 2015
9. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306;
10. Sheria ya Uhamiaji, SURA 54;
11. Sheria ya Ardhi, SURA 113;
12. Sheria ya Madini, SURA 123;
13. Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82;
14. Sheria ya Magari ya Kigeni, SURA 84;
15. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;
16. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196
17. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

### G. Vipaumbele vya kibajeti kwa Mtazamo wa Haki za Binadamu kwa mwaka wa Fedha 2023/2024

#### 1. Kuhusu mchakato wa uhuishwaji wa mchakato wa Katiba

Serikali ya awamu ya sita imeahidi mara nyingi kusudio lake la kufufua mchakato wa katika mpya.

Mapendekezo ya bajeti ya Serikali 2023/2024 haina fungu mahususi kwa ajili ya uhishisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba, pamoja na michakato ya mabaoresho ya sheria kama kipaumbele ndani ya bajeti hii. Sheria hizo ni kama, Sheria ya Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na Sheria ya Kura ya Maoni.

## 2. Haki ya Elimu

Pendekezo la kufutwa kwa ada kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kupangiwa na serikali kujiunga na vyuo vya ufundi kama DIT, Mbeya University of Science and Technology, na Arusha Technical College, mapendekezo haya yatasaida.

Pendekezo la kuanzishwa kwa programu ya mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa na serikali kusoma kwenye vyuo vinavyotoa elimu katika fani za kipaumbele ambazo ni, sayansi, afya, ufundi na ualimu, pendekezo hili litasaidia mamilioni ya watoto wengi masikini kufikia ndoto zao, hata hivyo tunatoa wito fursa hizi zitolewe kwa usawa na kuzingatia mahitaji na vipaumbele vya wanafunzi husika.

Ongezeko la posho ya kujikimu maarufu kama boom kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi 8, 500 mpaka shilingi 10,000 kwa siku, hatua hii itasaidia vijana wengi wa watoto masikini kutimiza ndoto zao za elimu, hata hivyo, tunatoa wito vigezo vya utoaji wa mikopo hiyo vitolewe kwa usawa.

Kufutwa kwa ada ya shule kwa wanafunzi wa kidato cha nne mpaka cha sita.

## 3. Haki ya kiuchumi na mawasiliano

Mapendekezo ya bajeti yanalenga kufuta tozo kwa siku kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji ili kuchochea matumizi ya kielektroniki katika miamala mbalimbali.

Kwa upande mwingine, bajeti inapendekeza kuondozo tozo ya miamala ya fedha zinazotumwa kwa njia ya simu, hata hivyo, bajeti inapendekeza kuongeza tozo hiyo kwa asilimia 50% wakati wa kutoa fedha.

## 4. Gharama za Maisha

Hotuba ya bajeti inapendekeza kuongeza tozo ya **shilingi 100** kwa lita ya petroli na dizeli kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati. Ikumbukwe kwamba, Serikali kutoa ruzuku ya shilingi **bilioni 479**.4 katika mafuta ya petroli na dizeli ili kupunguza ukali wa maisha, kwa mshangao bajeti hii inapendekeza kuongeza tozo kwenye mafuta ambayo kimsingi ni bidhaa inayotegemewa na sekta zote za kiuchumi na uzalishaji mali.

## 5. Haki ya Afya bora

Hotuba ya bajeti hii imeeleza kuwa Serikali imejipanga kulipa madeni inayodaiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), hatua hii itaongeza ufanisi wa Mfuko huo kwa kuwa unakumbwa na changamoto kubwa ya kifedha.

Serikali inapendekeza kusamehe Kodi ya Mapato kwenye mapato yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwenye amana (fixed deposit), hati fungani za muda mfupi (treasury bonds and treasury bills) pamoja na gawio linalotokana na hisa.

## 6. Haki ya kufanya kazi na kulipwa ujira unaostahili

- Kupandisha madaraja watumishi 135, 170 wenye sifa stahiki.

- Kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, ambapo kima cha chini cha mshahara kiliongezeka kutoka shilingi 300,000/= hadi shilingi 370,000/=, pendekezo hili linaendana na mikataba ya kimataifa ya shirika la kimataifa la kazi pamoja na mikataba mingineyo ya kimataifa inayozungumzia haki za kufanya kazi na kulipwa ujira unaostahili.

- Kulipa madeni ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 94,290 yenye thamani ya shilingi bilioni 165.9 hadi Aprili 2023.

- Kupunguza kodi ya mapato ya ajira (PAYEE) kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8%.

Hatua hii inaendana na misingi mbalimbali ikiwemo mikataba ya kimataifa ikiwemo ile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) inayosisitiza nchi wanachama wa mikataba a hiyo kupandisha madaraja watumishi wa umma pamoja na ongezeko la mishahara kwa kila mwaka.

## 7. Haki za Binadamu na Biashara

Bajeti inapendekeza kuweka mazingira wezeshi kwa biashara kwa kuweka zuio la kufungwa kwa biashara, ofisi au maeneo yoyote ya uzalishaji kwa sababu za kukiuka taratibu mbalimbali, badala yake hatua hizo zichukuliwe kwa mtu binafsi mwenyebiashara hiyo kwa makosa ya kibiashara na siyo kufunga biashara.

Hii ni hatua nzuri yenye lengo la kukuza biashara, hata hivyo LHRC ina maoni ya kuwa, pamoja nia hiyo nzuri, ni

muhimu kuzingatia ulinzi wa haki za walaji, kwa kuwa taasisi za udhibiti ni vyombo muhimu vya usalama wa bidhaa na hazi za walaji “Consumer protection”.

## H. Mapendekezo ya jumla

1. Kuainisha mchakato wa katiba miongoni mwa vipaumbele vya bajeti ya Serikali 2023/24.

2. Kuainisha suala la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama moja ya vipaumbele vya bajeti.

3. Kwa uzoefu tuliopata kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mambo mengi kupachikwa kwenye kanuni badala ya sheria mama hatua zilizopelekea LHRC kungua kesi ya kikatiba mahakama kuu, tunapendekeza kwa bunge kuhakikisha kwamba kilichopendekezwa na waziri kinakuwa kwenye sheria mama ya fedha 2023.

4. Kuhakikisha kwamba Kanuni zote za fedha zinapitiwa na kamati ya kudumu ya bunge ya sheria ndogo ili kuondoa uwezekano wa malalamiko na uzoefu tulioupata mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo kanuni zilizoanzisha tozo za miamala ya kielektroniki zilitungwa huku wabunge walio wengi wakilalamika kutoshirikishwa katika mchakato huo.

5. Tunapendekeza kupunguzwa kwa kodi ya mapato ya ajira( PAYEE) kutoka asilimia 8 ya sasa mpaka asilimia 6%.

6. Sheria zote 17 zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho na Mswaada wa Fedha kwa mwaka 2023/2024 ziendane na mapendekezo ya bajeti kuu.


LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU
TANZANIA
BAJETI YA SERIKALI
2023/24